

Udhibiti wa bungua viazi kwa kutumia marejea

Tambua tatizo

Bungua wa viazi vitamu ni wadudu waharibifu wa mizizi ya viazi vitamu. Bungua huwa na urefu wa milimita 6 na mwili mwembamba unaong'ara na pua ndefu. Miguu na kichwa cha bungua huwa na rangi nyekundu na sehemu nyingine za mwili huwa na rangi ya bluu -nyeusi. Mabuu ni hatua ya ukuaji wa bungua ambayo ndiyo hugaribu viazi. Mabuu huwa na urefu wa milimita 2 hadi 6, na umbo la C. Mabuu huwa hayana miguu na huwa na rangi nyeupe inayoelekea kuwa kijivu.


Habari tangulizi

Bungua hutaga mayai karibu na shina la kizazi. Mayai huanguliwa na kuwa mabuu. Mabuu hushambulia viazi na kusababisha mashimo yenye rangi nyeusi, viazi kuwa na hali ya sponji hivyo kuvifanya kukosa soko. Bungua wanaweza kuathiri viazi vikiwa shambani na wakati wa kuhifadhi. Viazi vilivyoshambuliwa huwa ladha chungu na harufu mbaya. Hasara kutokana bungua wa viazi vitamu huwa kati ya asilimia 2 hadi 97. Marejea ni mimea jamii ya kunde yenye uwezo wa kufukuza bungua wa viazi vitamu shambani. Matumizi ya marejea hayaathiri mavuno ya viazi. Yana faida pia katika kuzuia ukuaji wa magugu na huboresha rutuba ya udongo.


Usimamizi

- Panda viazi vitamu katika matuta yaliyoandaliwa vizuri yenye kimo cha sentimeta 30 na upana wa sentimeta 60.
- Mbegu za marejea zinaweza kupatikana sehemu mbalimbali mfano kutoka Benki ya Mbegu za Marejea, Sanduku la Posta 1, Peramiho, Tanzania. Mbegu za marejea zilizovunwa msimu uliopita zinaweza kuhifadhiwa na kutumika misimu mingine.
- Sambaza na kufukia mbegu za marejea kwenye matuta ya viazi vitamu mwezi 1 baada ya kupanda viazi. Kilo arobaini za mbegu hutosha hekta 1
- Marejea yakiota kwa wingi, punguza miche kwa nafasi ya kati ya sentimeta 30 hadi 40 kati ya mmea na mmea.
- Acha marejea yakue pamoja na viazi hadi wakati wa kuvuna viazi.
- Kata marejea na vuna mbegu kabla ya kuvuna inafanywa
- Epuka kuhifadhi viazi vilivyoshambuliwa na bungua ili kuzuia mashambulizi zaidi wakati wa kuhifadhi

(a) Mabuu ya bungua na (b) bungua pevu. (Picha na (a) James Castner, (b) EcoPort)



(a) Kizazi kilichoshambuliwa (b) mmea wa marejea. (Picha na (a) Vilma Amante (b) Nathan Siemers)



Jina la kisayansi > *Cylas formicarius*

Mapendekezo katika vidokezo hivi yanatumika katika: Tanzania



WAANDISHI: Hosea D Mtui, Rose Ndomba, Jubilant JN Mwangi
Sokoine University of Agriculture
Barua pepe: mtuihosea@yahoo.com

Mwisho na Plantwise